



The Human Rights Centre Uganda



**AZIMIO LA KIMATAIFA JUU YA HAKI ZA KIBINADAMU SURA YA
NNE YA KATIBA YA JAMHURI YA UGANDA YA 1995:
MASIMULIZI YALIYOFASIRIWA KWA URAHISI NA KUFUPISHWA**

UTANGULIZI

Sura ya nne ya katiba ya Jamhuri ya Uganda ya 1995, ina haki za kimsingi za kibinadamu, na uhuru unaowastahiki binadamu wote. Sura ya 4 ya katiba ya Jamhuri ya Uganda ya 1995, ina haki za kimsingi za kibinadamu, zinazowastahili binadamu wote. Hizo ni haki za kimsingi kwa walimwengu wote, zikiwa za umuhimu kwa usawa na uwiano. Kijitabu hiki, ni cha kwanza kwa matoleo ya Kituo cha Shirika la Haki za kibinadamu la Uganda, ambacho kimefasiriwa/kimetafsiriwa kwa lugha za kienyeji zinazozungumzwa sana nchini Uganda. Lugha hizo ni: Acholi, Ateso, Kiswahili, Lango, Luganda, Runyankore, Rukiga, Runyoro na Rutooro. Kituo hiki cha haki za Kibinadamu kinafahamu/tambua tafsiri za aina mbalimbali zilizofanywa na mashirika mengine kuhusu Katiba, na kimefanya juhudi zaidi kwa kurahisisha na kufupisha maazimio yaliyomo kwenye Sura ya Nne.

Kituo hiki kinalenga kuwapasha taarifa umma kuhusu uhuru na haki zao za kimsingi, huku tukikuhimiza usambaze taarifa kama uwezavyo.

Pongezi maalumu zifikie Ubalizi wa Ufalme wa Norway, na shirika la "Irish Aid" kwa misaada ya kifedha, iliyowezesha uzalishaji wa kijitabu hiki. Kituo hiki pia kinatoa pongezi kwa Tume ya Kurekebisha Sheria ya Uganda (Uganda Law Reform Commission), kwa misaada yake ya kiufundi kwa kurahisisha na **kufupisha** Sura ya Nne.

JUA HAKI ZAKO, SEHEMU YA 1

Sehemu ya 4 ya Katiba ilyofanyiwa marekebisho

Kifungu 20

1. Watu wote tumezaliwa huru, tuna haki sawa na heshima sawa. Haki zetu hazitokani na serikali au nchi yoyote.
2. Haki zangu na uhuru wangu, lazima viheshimiwe na vilindwe na serikali, vyombo vyote vya serikali na watu wote.

Kifungu 21.

1. Niko sawa mbele ya sheria na nina haki za kulindwa na sheria.
2. Sistahili kubaguliwa au kubagua mtu yoyote kutokana na kabila, jinsia, rangi, mahali pa kuzaliwa, dini, mazingira, siasa, ulemavu, jamii na hali ya uchumi.
3. Bunge lazima lipitisha sheria za kuondoa ubaguzi na unyanyasaji kwenye jamii yetu.

Kifungu 22.

1. Nina haki ya kuuishi na haki hiyo haitolewi ila kupitia sheria ya kifo ilyopitiswa na kuhakikiswa na mahakama iliyokubalika.
2. Utoaji wa mamba ni marufuku hadi sheria iruhusu.

Kifungu 23

1. Mtu hawezi kukamatwa au kuwekwa jelani hadi sheria zulizotungwa kwenye katiba zitumike.
2. Mtu akikamatwa au mtu akifungwa, lazima aelezwe sababu za kukamatwa kwake, awekwe mahali panaporuhusiwa na sheria na apelekwe mahakamani kwenye muda wa masaa arobaini na nane/manane.
3. Mtu yoyote akipelekwa mahakamani kwa ajili ya kosa, anaweza kupewa rufani ikiwa mahakama itakubali.

4. Mtu yoyote akikamatwa au kufungwa bila makosa yoyote, atapewa fidia ya kufungwa au kukamatwa bila kosa.

Kifungu 24.

1. Hakuna mtu yoyote anayeruhusiwa kuumiza mtu yoyote kimawazo, kumpiga mtu yoyote au kumnyanyasa mtu yoyote.

Kifungu 25.

1. Hakuna mtu yoyote atakayefanya mtumwa au kuishi kwenye utumwa.
2. Hakuna mtu yoyote atayefanyishwa kazi kwa nguvu ila kwa sababu zifuatazo;
 - i. Ikiwa ni uamuzi wa mahakama inayokubalika.
 - ii. Ikiwa ni kazi kwenye gereza kwa ajili ya usafi au kuendeleza sehemu alipofungwa mtu.
 - iii. Ikiwa ni kazi ya Askari wa jeshi linalohusika.
 - iv. Ikiwa ni kazi wakati wa kipindi cha dharura au wakati wa maafa.
 - v. Ikiwa ni kazi inayoruhusiwa kwenye jamii au mazingira.

Kifungu 26.

1. Kila mtu ana haki ya kumiliki mali na vitu, kumiliki pekee yake au kumiliki na watu wengine.
2. Mali ya mtu haiwezi kuchukuliwa isipokuwa kwenye hali ifuatayo:
 - i. Mali ikitakiwa kwa ulinzi wa nchi, matumizi ya umma, usalama kwa jumla, ulinzi wa tabia nzuri kwenye jamii au kwa afya ya jamii.

JUA HAKI ZAKO, SEHEMU YA 1

- ii. Mali ya mtu itatumiwa baada ya kumpa fidia ya mali hiyo.
3. Hakuna sheria itakayomkataza mtu kushitaki na kwenda mahakamani ikiwa mali yake na vitu vyake vitachukuliwa kwa nguvu.

Kifungu 27

Sote tuna haki ya ulinzi wa miili yetu, nyumba zetu na mali yetu; na vitu hivyo havikaguliwi bila ruhusa. Nyumba zetu na mali na vitu vyetu havikaguliwi bila ruhusa na haviingiwi bila ruhusa.

Kifungu 28.

1. Watu wote tuna/Nina haki ya kusikilizwa mahakamani na hukumu halali kutolewa na mahakama inayokubalika kisheria na bila kuchelewesha kesi na unafuu wa kusikilizwa.
2. Mtu yoyote anaposhitakiwa kwa kufanya kosa, yafuatayo huzingatiwa:
 - i. Mtu hana kosa mpaka apatikane na hatia.
 - ii. Mtu lazima afahamishwe kosa alilofanya kwenye lugha anayoifahamu.
 - iii. Lazima mtu apewe muda wa kujitetea.
 - iv. Mtu aruhusiwe kwenda mahakamani na kupata hakimu.
 - v. Mtu ana haki ya kupata huduma za hakimu wa Taifa ikiwa ameshitakiwa kwa kosa la jinai kama vile kifo au kufungwa maisha.
 - vi. Mtu ana haki ya kutumia Mkalimani mahakamani ikiwa mtu huyo hafahamu lugha inayotumiwa mahakamani.
 - vii. Mtu ana haki ya kusaidiwa na mashahidi wake na kuwauliza

maswali mashahidi wa upande unaomshitaki.

3. Mtu akishitakiwa kwa kufanya kosa, lazima awepo wakati wa kesi inapofanyika, isipokuwa mahakama ikimkataza kuwepo kwenye kesi kwa sababu za tabia ya mtu huyo kuweza kudhorotesha kesi hiyo.
4. Mtu hawezi kutiwa kwenye hatia ya kufanya kosa la jinai ikiwa halikuwa kosa la jinai wakati alipotenda kosa hilo.
5. Mtu hawezi kushitakiwa kwa kosa la jinai ikiwa alisamehewa kosa hilo kulingana na sheria.
6. Mtu hawezi kushitakiwa tena kwa kosa alilosamehewa au kwa kesi aliyoshinda isipokuwa mahakama kuu ikiamrisha kurudiwa kwa kesi hiyo.
7. Makosa yote lazima yawe kwenye sheria, Mtu hawezi kuwekwa hatiani kwa kosa ambalo haliko kwenye sheria, isipokuwa mahakama ikitoa uamuzi huo.
8. Mke au mume wa mtu hatalazimishwa kutoa ushahidi dhidi ya mwenzake kwenye makosa ya jinai.

Kifungu 29.

Watu wote wana haki zifuatazo;

- i. Haki ya uhuru wa mawazo na uhuru wa kuabudu na ibada.
- ii. Uhuru wa kuongea na kujieleza.
- iii. Uhuru wa kutenda na kuabudu kwenye dini ya uamuzi wake kulingana na katiba ya nchi.

JUA HAKI ZAKO, SEHEMU YA 1

- iv. Uhuru wa kukutana na kuandamana kwa amani.
- v. Uhuru wa kujiunga na mashirika na kujiunga kwa vyama vya siasa.
- vi. Uhuru wa kusafiri na kuishi mahali popote nchini Uganda.
- vii. Uhuru wa kuingia, kutoka na kurudi nchini Uganda.
- viii. Haki ya kuwa na Pasipoti na haki ya kuwa na vyeti vya kusafiria.

Kifungu 30.

Wote tuna haki ya kupata elimu.

Kifungu 31.

1. Watu wote wenye miaka 18 na zaidi wana haki ya kuoza, kuolewa na kuanzisha familia.
2. Ndoa za watu wenye jinsia moja ni marufuku na hazikubaliki kisheria.
3. Ndoa ni makubaliano kati ya mwanamme na mwanamke.
4. Mume na mke wana haki sawa wakati wakioana, wakati wa ndoa na wakati wanapoachana. Haki juu ya watoto na haki juu ya mali na kadhalika.
5. Ni jukumu la wazazi wawili kuwatunza, kuwahudumia na kuwakuza watoto wao.
6. Watoto hawatatenganishwa na wazazi wao au na walinzi wao ila kwa sheria.
7. Bunge lazima litunge sheria za kuwalinda wajane na wajane wa kiume kuhusu mali ya waliokufa, walio oana na watoto waliobaki.

Kifungu 32.

1. Taifa lazima liboreshes hali ya watu wenye matatizo ya kimaumbile kulingana na miaka yao, jinsia, ulemavu, historia na mila na utamaduni wao.
2. Sheria yoyote ile, mila na utamaduni vinavyonyanyasa maendeleo ya wanawake au maendeleo ya watu wa kikundi Fulani ni marufuku na imekatazwa kwenye katiba.

Kifungu 33.

1. Wanawake wote wamezaliwa huru na haki sawa kama wanaume.
2. Taifa lazima liendeleze na litoe nafasi ya maendeleo ya wanawake.
3. Taifa lazima lilinde wanawake na lilinde haki za wanawake kwa kuzingatia hali yao ya uzazi na kuzaa.
4. Wanawake wana haki kama za wanaume na wapewe usawa kwenye shughuli za siasa, uchumi na jamii.
5. Wanawake wana haki ya kupinga unyanyasaji kutokana na historia, mila na utamaduni wetu.

Kifungu 34.

1. Watoto wote wana haki ya kuwajua wazazi wao, kulelewa na wazazi wao au kulelewa na walinzi wao.
2. Taifa na wazazi wa watoto wana jukumu la kuwapa elimu watoto wote.
3. Hakuna mtu yoyote atakayenyima mtoto huduma ya matibabu, elimu, au huduma yoyote kwa ajili ya diini au imaani yake.
4. Hakuna mtoto atakayetumiwa vibaya kiuchumi, kufanyishwa kazi zinazolingiliana na elimu ya mtoto, au kazi inayodhuru afya

JUA HAKI ZAKO, SEHEMU YA 1

ya mtoto huyo, kazi inayodhuru akili ya mtoto au kazi inayodhuru hali ya maisha ya kawaida na maendeleo ya mtoto.

5. Watoto yatima wote na watoto wenye matatizo ya kimaumbile wana haki ya kulindwa na Taifa.
6. Mtoto mhalifu hafungwi kwenye jela na watu wakubwa.

Kifungu 35

1. Walemavu wote wana haki ya kuheshimiwa na haki ya kutendewa utu.
2. Taifa litahakikisha kwamba walemavu wote wanatumia na kuendeleza vipaji vyao.

Kifungu 36.

1. Watu wa hali ya chini wana haki ya kushiriki kwenye ngazi za kuchukua uamuzi. Mipango ya Taifa izingatie mawazo an fikra ya watu hao.

Kifungu 37.

1. Una haki ya kuhusika, kutenda na kuendeleza mila zako, lugha zetu, utamaduni, imani au diini kibinafsi au kwa pamoja na wengine.

Kifungu 38.

1. Una haki ya kuchagua Serikali na kushiriki kwenye mipango ya Serikali kwa binafsi au kwa kupitia wajumbe tuliowachagua.
2. Una haki ya kuelekeza mipango ya Serikali kwa kupitia vitendo vya amani au kupitia vitendo vya mashirika ya umma.

Kifungu 39.

1. Una haki ya mazingira safi na mazingira salama kwa afya yetu.

Kifungu 40.

1. Una haki ya kufanya kazi na kufanya kazi kwenye mazingira masafi na mazuri.
2. Una haki ya kupumuzika na kupata mapumziko ya kazi yanayolipwa.
3. Una haki ya kutumia elimu uliyopata na tunaruhusiwa kufanya kazi halali na kufanya biashara halali.
4. Kila mfanyakazi ana haki ya kuwa kwenye chama cha biashara cha uamuzi wake na kushiriki kwa jumla kulinda malengo yake ya uchumi.
5. Kila mfanyakazi ana haki ya kujiuzulu au kukataa ajira kulingana na sheria.
6. Wanawake wajawazito ambao ni wafanyakazi wana haki ya kulindwa na waajiri wao wakati wa uja uzito na baada ya kujifungua.

Kifungu 41.

Una haki ya kupata habari zilizohifadhiwa na Serikali isipokuwa habari hizo zikiwa zitaathiri ulinzi wa Taifa au ku kudhuru haki ya mtu mwingine.

Kifungu 42.

Una haki ya kutendewa sawa na maafisa wa utawala au vyombo vya utawala na tuna haki ya kupinga uamuzi wa vyombo hivyo mahakamani.

Kifungu 43.

1. Ni jukumu lako kuheshimu haki za wengine na kulinda haki zetu kwa kutoingilia haki za wengine au kuingilia haki za umma.
2. Kutumia haki zetu kunaweza kuwa na mipaka kwa ajili ya manufaa ya umma, lakini mipaka hiyo hayihusiani na:

JUA HAKI ZAKO, SEHEMU YA 1

- i. Unyanyasaji wa kisiasa.
- ii. Kufungwa bila kesi mahakamani.
- iii. Kufanyika kwa kitendo chochote ambacho hakikubaliki kwenye umma au kitendo chochte ambacho hakikubaliki kwenye katiba.

Kifungu 44.

Kwa namna yoyote haki zifuatazo haziwezi kutolewa:

- i. Uhuru wa kutoadhibiwa, haki ya kutoteswa, na haki ya kutoondolewa hadhi.
- ii. Uhuru wa kutokuwa mtumwa au kutokuwa kwenye utumwa
- iii. Haki ya kutosikilizwa kikamilifu.
- iv. Haki ya kuomba mahakama kupelekwa mahakamani ili kupinga kufungo unachokitumikia.

Kifungu 45.

Unaruhusiwa kuwa na haki za Binadamu na haki za uhuru kama iliyotajwa kwenye Katiba na unaruhusiwa haki zote ambazo hazikutajwa kwenye Kaiba ya nchi.

Kifungu 46.

1. Bunge linaweza kupitisha sheria ya kuruhusu sheria Fulani zitungwe kwenye wakati wa kipindi cha dharura kwa kuwafunga watu Fulani kwenye kipindi cha dharura.

Kifungu 47.

Ikiwa mtu yoyote atafungwa chini ya sheria za kipindi cha dharura lazima:

- i. Mtu huyo atafahamishwa kwa maandishi sababu zilizomfanya afungwe kwenye kipindi kisicho zidi saa 24.
- ii. Mke au mume au mtu anayehusiana na mfungwa yoyote atafahamishwa kwenye kipindi cha saa 72.
- iii. Tangazo la kumfunga mtu litatolewa kwenye gazette ya Serikali kwenye kipindi cha siku 30 na kuelezea sababu za kufungwa mtu huyo na sheria iliyotumika.

Kifungu 48.

1. Tume ya Uganda ya haki za Binadamu lazima itazame kesi ya mtu aliyefungwa chini ya sheria za kipindi cha dharura kwenye muda wa siku 21 na kila baada ya siku zisozozidi kipindi cha siku 30.
2. Tume ya Halmashauri ya haki za Binadamu inaweza kuamrisha kuachiliwa kwa mtu aliyefungwa chini ya sheria za kipindi cha dharura au kupinga kukamatwa au kufungwa mtu huyo.
3. Mtu aliyefungwa chini ya sheria za kipindi cha dharura ana haki ya kupelekwa mbele ya Kamisheni ya haki za binadamu au kuwakilishwa na wakili wakati kesi yake inapokuwa inaangaliwa upya.

Kifungu 49.

1. Serikali ikitangaza kipindi cha dharura nchini lazima ifahamishe Bunge na Serikali itangaze habari ya dharura kila mwezi, asaerikali itangaze yafuatayo:
 - i. Majina na idadi ya watu waliofungwa kwa kipindi hicho.

JUA HAKI ZAKO, SEHEMU YA 1

- ii. Hatua zipi zilizochukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na Kamisheni ya haki za Binadamu.
 - iii. Idadi ya kesi zilizishuhuliwa na Kamisheni ya haki za Binadamu.
2. Wakati wa mwisho wa kipindi cha dharura kilicho kubaliwa na katiba, watu wote waliofungwa wataachiliwa isipokuwa mtu mwenye kosa la ziada.

Kifungu 50.

1. Una wajibu wa kesi yako kusikilizwa upya mahakamani ikiwa haki zetu kwenye katiba zimekiukwa na kesi zetu kupelekwa mahakamani.
2. Mtu yoyote au kikundi chochote kina haki ya kutetea haki ya mtu mwingine au haki ya kikundi chochote kingine.
3. Bunge lazima litunge sheria za kuongezea nguvu haki za Binadamu na uhuru wa kimsingi.

Kifungu 53.

Haki zako zikikiukwa, unaweza kutowa malalamiko yako kwenye Kamisheni ya Uganda ya haki za Binadamu ambayo ina amri ya kufanya mabadiliko na kuangalia kesi yako upya.

The Human Rights Centre Uganda,
P. O. Box 25638, Kampala,
Uganda.

Telephone: +256 414 266186
E-mail: hrcug@hrcug.org
Website: www.hrcug.org